

**MAAMBUKIZI YA TB YASIYO  
NA MADHARA.**

**HATARI YA UWEZEKANO WA  
KUSHIKWA NA UGONJWA.  
MWONGOZO WA WAGONJWA**

Mpango wa Kifua Kikuu  
Idara ya Afya ya Virginia

Nyenko hii ya wagonjwa inalenga kutoa taarifa kuhusu maambukizi ya TB yasiyo na madhara (LTBI), ikiwa ni pamoja na historia ya maambukizi hayo, jinsi yanavyotambuliwa, na yanavyotibiwa. Ingawa nyenko hii ilibuniwa ili kuwa ya manufaa kwa wagonjwa wote, tunatumai kwamba itakuwa na umuhimu zaidi kwa wale walioambukiziwa TB, wale walio ambukiziwa TB, wale wanaofanya kazi katika mazingira yenye hatari kubwa ya kuambukiziwa TB, pamoja na jamaa, marafiki, na watu wengine walio karibu nao.


Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu hapa  
<https://www.vdh.virginia.gov/tuberculosis/>.

# I. USULI

## MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA (LTBI) NI NINI?

Maambukizi ya TB yasiyo na madhara (LTBI) ni hali ambapo watu huambukizwa bakteria inayosababisha kifua kikuu (TB), lakini hawaugui kama wale walio na ugonjwa amilifu wa TB.

Maambukizi ya TB yasiyo na madhara yanayo julikana wakati mwingine kama "TB iliyodumaa", ni bakteria za TB zilizo katika mwili lakini sio amilifu, na hazikui. Kwa sababu kinga ya mwili ina uwezo wa kupambana na bakteria za TB, mtu mwenye maambukizi ya TB yasiyo na madhara hana dalili zozote, hajisikii mgonjwa, na hawezi kueneza bakteria za TB kwa wengine.




TB ni ugonjwa unaoweza kuzuilia na kutibika unaosababishwa na bakteria inayoitwa *Mycobacterium tuberculosis* (*M. tuberculosis*). Hata hivyo, sio kila mtu ambaye anaambukizwa bakteria ya *M. tuberculosis* hushikwa na ugonjwa amilifu wa TB. Bakteria hii kwa kawaida hushambulia mapafu, lakini inaweza kudhuru sehemu yoyote ya mwili. Dalili zinaweza kuwa tofauti kulingana na mahali ugonjwa huu unaposhambulia mwili. Dalili hizi zinaweza kuwa ni pamoja na kikohozi kinachodumu zaidi ya wiki 3, udhaifu wa mwili, homa, kutokwa na jasho usiku, maumivu ya kifua, na kukohoa damu. Ugonjwa amilifu wa TB usipotibiwa unaweza kusababisha kifo.

Ijapokuwa kwamba ukiwa na maambukizi ya TB yasiyo na madhara hizo bakteria sio amilifu, zinabakia hai katika mwili wako na zinaweza kuwa amilifu zisipotibiwa. Hii ikitokea, unaweza kupata ugonjwa amilifu wa TB, ambao utakufanya uwe mgonjwa sana. Kwa hivyo, ni muhimu sana kukamilisha matibabu ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara ili kujikinga dhidi ya kupata ugonjwa amilifu wa TB.

## WATU HUPATA MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA VIPI?

Bakteria za TB huenea kuitia hewa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine wakati mtu ambaye anaugua ugonjwa amilifu wa TB anaongea, kukohoza, kucheka, kuimba, au kupiga chafya. Bakteria za TB zinaweza kuachiliwa hewani na ikiwa umekaribiana na mtu huyu wakati hili linatokea, unaweza kuvuta ndani hewa yenye bakteria hizi na kuambukizwa.

Ugonjwa amilifu wa TB huenea sana mionganoni mwa watu ambao wanaukutana kila siku na kutangamana kwa karibu - kama vile wanafamilia, marafiki, wafanyakazi wenza, au wanafunzi wenza.



Ikiwa ulizaliwa nje ya Marekani, huenda umepokea chanjo ya bacille Calmette-Guérin (BCG) ulipokuwa mtoto. Chanjo hii inazuia watoto wachanga na wadogo dhidi ya kupata aina kali za ugonjwa wa kifua kikuu. Hata hivyo, haikupi kinga ya maisha yako yote dhidi ya TB. Angalia Sehemu ya II ili ujifunze jinsi unavyoweza kufanyiwa vipimo vya TB hata kama ulipokea chanjo ya BCG utotonu wako.

## NI NANI ALIYE KATIKA HATARI YA KUPATA UGONJWA AMILIFU WA TB?

Ingawa ni 5-10% tu ya watu walio na maambukizi ya TB yasiyo na madhara watakaoshikwa na ugonjwa amilifu wa TB ikiwa maambukizi hayo hayatatibiwa, takriban 80% ya visa vya ugonjwa amilifu wa TB nchini Marekani hutokana na maambukizi ya TB yasiyo na madhara yasiyotibiwa. Aidha, baadhi ya watu walio na maambukizi ya TB yasiyo na madhara wana uwezekano mkubwa wa kushikwa na ugonjwa amilifu wa TB kuliko wengine.

### HUWEZI KUPATA KIFUA KIKUU KWA:

- Kushiriki vyakula au vinywaji na watu wengine
- Kusalmiana kwa mikono
- Kukumbatiana
- Kugusa viti vya choo

Watu walio katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa amilifu wa TB kwa ujumla huwa katika makundi mawili:


1. Watu waliaoambukizwa bakteria ya TB hivi karibuni (ndani ya miaka miwili tangu wakati wa kuambukizwa);
2. Watu wenye hali zifuatazo, ambazo hudhoofisha mfumo wa kinga:
  - Maambukizi ya virusi vya UKIMWI
  - Matumizi ya dawa za kulevyta, hasa dawa za kujidunga sindano
  - Matibabu maalum ya ugonjwa wa baridi yabisi au ugonjwa mfumo wa kumeng'anya chakula wa Crohn's
  - Upandikizwaji wa viungo vya mwili
  - Ugonjwa sugu wa figo
  - Saratani ya kichwa na shingo
  - Kisukari
  - Matibabu, kama vile matumizi ya dawa za kutibu uvimbe
  - Ugonjwa wa mapafu wa Silicosis
  - Uzito wa chini wa mwili
3. Aidha, watoto, hasa wale walio chini ya umri wa miaka mitano, wana hatari kubwa ya kupata ugonjwa amilifu wa TB wanapoambukizwa.

## II. VIPIMO

### JE, NINAPASWA KUFANYIWA KIPIMO CHA TB?

Unapaswa kupimwa ikiwa:

- Umetumia muda na mtu anayejulikana au kushukiwa kuwa na ugonjwa amilifu wa TB;
- Una dalili za ugonjwa amilifu wa TB;
- Ulizaliwa, umeishi, au umesafiri mara nyingi katika nchi ambazo zina visa vingi vya ugonjwa amilifu wa TB;
- Una VVU au hali nyingine ambayo inadhoofisha mfumo wako wa kinga;
- Unatumia dawa za kulevyta kwa njia ya sindano;
- Unafanya kazi au kuishi katika mazingira yenye watu wengi ambapo kuna visa vingi vya maambukizi ya kifua kikuu, kama vile makazi ya muda mfupi kwa wasio na nyumba, taasisi za marekebisho ya tabia, au makazi ya kutunzia wakongwe na walemaavu.



### NITAFANYIWAJE KIPIMO CHA MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA?

Kuna chaguzi mbili za vipimo vya maambukizi ya TB yasiyo na madhara - kipimo cha damu cha TB na kipimo cha ngozi cha TB. Unaweza kupata kipimo cha ngozi au damu cha TB kutoka kwa daktari wako au idara ya afya ya mtaa wako. Mto huduma wako wa afya atakueleza ni kipimo gani kinachokufaa zaidi, na unapaswa kupanga kurudi tena kwa utunzaji zaidi ikiwa imetambuliwa kuwa una ugonjwa amilifu wa TB au maambukizi ya TB yasiyo na madhara.

### VIPIMO VYA DAMU VYA KIFUA KIKUU

Vipimo vya damu vya kifua kikuu, ambavyo pia hujulikana kama interferon gamma release assays (IGRAs), huhitaji utembelee mto huduma wako wa afya mara moja. Mto huduma wako atatoa sampuli ya damu yako na kuituma kwenye maabara ili kubaini ikiwa umeambukizwa bakteria

za kifua kikuu. Kipimo cha IGRA ndicho kipimo cha kifua kiukuu kinachopendelewa kwa wale ambao wamepokea chanjo ya BCG, na kwa wale ambao wanatatizika kurudi tena kuonana na mto huduma wa afya ili kufanyiwa kipimo cha ngozi cha kifua kikuu.

- Kipimo chanya cha IGRA humaanisha kuwa umeambukizwa bakteria za kifua kikuu. Hata hivyo, utahitaji vipimo vya ziada ili kubaini ikiwa una maambukizi ya TB yasiyo na madhara au ugonjwa amilifu wa TB.
- Matokeo hasi ya kipimo cha IGRA yanamaanisha kuwa kipimo hakikutambua maambukizi katika damu yako na kuna uwezekano mdogo kwamba una maambukizi ya TB yasiyo na madhara na ugonjwa amilifu wa TB.

## VIPIMO VYA NGOZI VYA TB

Sawa na kipimo cha damu cha kifua kikuu, kipimo cha ngozi cha TB au (TST) ni kipimo kinachofanywa na mtoe huduma wako wa afya ili kubaini ikiwa umeambukizwa bakteria za TB. Katika kipimo hiki, mtoe huduma wako wa afya atakudunga kiasi kidogo cha tuberculin, ambayo ni protini ya upimaji, katika sehemu ya chini ya mkono wako. Kisha, baada ya saa 48-72, utarudi kwa mtoe huduma wako wa afya ili kupima athari zozote ambazo huenda zimetokea katika sehemu ambapo tuberculin ilidungwa. Kulingana na matokeo ya kipimo cha athari yoyote na historia yako ya afya, mtoe huduma wako wa afya atabaini ikiwa matokeo ya kipimo ni chanya au hasi.

- Kipimo cha TST kilicho na matokeo chanya kinamaanisha kuwa umeambukizwa bakteria za TB. Hata hivyo, utahitaji vipimo vya ziada ili kubaini ikiwa una maambukizi ya TB yasiyo na madhara au ugonjwa amilifu wa TB.
- Kipimo cha TST kilicho na matokeo hasi kinamaanisha kwamba kipimo hakikutambua maambukizi katika mwili wako na kuna uwezekano mdogo kwamba una maambukizi ya TB yasiyo na madhara na ugonjwa amilifu wa TB.


## VIPIMO VYA ZIADA

Ikiwa umeambukizwa TB hivi karibuni, huenda ukahitaji kipimo cha pili cha TB wiki 8-10 baada ya kuambukizwa kwako, kwa kuwa bado inaweza kuwa mapema sana kwa mwili wako kutoa matokeo chanya. Ikiwa matokeo ya kipimo cha pili ni hasi, basi huenda huna maambukizi ya TB yasiyo na madhara na ugonjwa amilifu wa TB.

Ikiwa una ugonjwa amilifu wa TB, huenda ukafanyiwa kipimo cha virusi vya UKIMWI ili kubaini hali yako ya VVU. Hii ni muhimu kwa ajili ya matibabu na utunzaji wako.

Ikiwa matokeo yako ya vipimo vya IGRA au TST ni chanya, mtoe huduma wako wa afya atahitaji kufanya vipimo vya ziada ili kubaini kama una maambukizi ya TB yasiyo na madhara au ugonjwa amilifu wa TB. Hii kwa kwa kaida hujumuisha picha ya eksirei ya kifua ili kutafuta dalili za ugonjwa amilifu wa TB katika mapafu yako, lakini pia inaweza kujumuisha kupima sampuli ya kohoz ikiwa unakoho. Kwa kuwa maambukizi ya TB hayawi kwenye mapafu yako tu kila wakati, mtoe huduma wako wa afya anaweza pia kuchukua sampuli zingine.

Tafadhalii kumbuka kwamba, maambukizi ya TB yasiyo na madhara na ugonjwa amilifu wa TB ni hali zinazofaa kuripotiwa katika Virginia, kwa hivyo mtoe huduma wako wa afya atahitaji kuripoti matokeo yoyote chanya kwa idara ya afya ya eneo hilo. Hata hivyo, matokeo haya ya vipimo yatabaki siri, na hayatasababisha ufukuzwe kazi, au kuleta athari zozote kwa hali yako ya uhamiaji.



### III. MATIBABU

Tunaelewa kuwa kupatikana na maambukizi ya TB yasiyo na madhara kunaweza kukuzidia na kukuacha na maswali mengi. Tunataka kukuhakikisha kuwa **maambukizi ya TB yasiyo na madhara yanaweza kutibiwa** na matibabu haya yanaweza kukuzuia kupata ugonjwa amilifu wa TB. Ingawa ugonjwa amilifu wa TB pia unawenza kutibiwa, ukishikwa nao, huenda utajihisi mgonjwa sana na unawenza kueneza TB kwa wengine. Kwa hivyo, kutibu maambukizi ya TB yasiyo na madhara kunaweza kuhakikisha kwamba wewe, jamaa, marafiki, na wafanyakazi wenzako wana afya nzuri na usalama.

#### MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA HUTIBIWA VIPI?

Unawenza kuchagua kati ya chaguzi kadhaa zinazopatikana za matibabu ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara. Mto huduma wako wa afya atashirikiana nawe ili kutambua chaguzi za matibabu zitakazokufaa zaidi kulingana na hali yako ya sasa ya afya na dawa zingine unazotumia.

Hivi sasa, mashirika ya Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) na Chama cha Kitaifa cha Wadhibiti wa Kifua Kikuu (NTCA) yanapendekeza matibabu ya

muda mfupi. Chaguzi hizi zinakuwezesha kukamilisha matibabu yako katika muda wa miezi mitatu au minne. Ikiwa chaguzi hizi hazifai, basi mto huduma wako wa afya atakuhitaji kutumia matibabu kwa muda wa miezi sita au

tisa. Hizi hapa ni baadhi ya chaguzi za matibabu ziilizopo:

- Miezi mitatu ya matumizi ya isoniazid mara moja kwa wiki pamoja na rifapentine (3HP)
- Miezi minne ya matumizi ya rifampin kila siku (4R)
- Miezi mitatu ya matumizi ya isoniazid kila siku pamoja na rifampin (3HR)
- Miezi sita au tisa ya matumizi ya isoniazid (6H au 9H, mtawalia)

Kama ilivyoelezwa katika sehemu za awali, kuna makundi ya watu walio katika hatari kubwa zaidi ya kushikwa na ugonjwa amilifu wa TB wanapoambukizwa. Hii ni pamoja na watoto wachanga, watoto wadogo, na watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Watu hawa wanawenza kupata matibabu ikiwa wameambukizwa TB, hata kama



matokeo ya vipimo vyao vya TB ni hasi, kwa sababu ya hatari kubwa walio nayo. Tafadhali jadili haya na mto huduma wako wa afya ikiwa wewe au mtoto wako yuko miongoni mwa watu hawa.

Tunatambua kuwa matibabu ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara huchukua muda mrefu kuliko matibabu ya maambukizi mengine mengi ya bakteria, kama vile nimonia, ambayo pengine ulikuwa nayo. Hii ni kwa sababu bakteria ya TB hukua polepole sana kukua kuliko bakteria zingine nyingi, na kwa hivyo inahitaji matibabu ya muda mrefu. Hata hivyo, matibabu ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara ni sahili na ya haraka zaidi kuliko matibabu ya ugonjwa amilifu wa TB. Kumbuka kwamba kutumia matibabu yako kikamilifu jinsi mto huduma wako wa afya alivyokuelekeza ndiyo njia ya pekee tu ya kuzuia maambukizi ya TB yasiyo na madhara yasigeuke kuwa ugonjwa amilifu wa TB.

#### NINAHITAJI KUJUA NINI KUHUSU MATIBABU YA MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA?

Kulingana na chaguo lako la matibabu, utatumia dawa kila siku au kila wiki. Ni muhimu sana kutumia dawa zako jinsi mto huduma wako wa afya alivyokuelekeza, ikiwa ni pamoja na kutumia dozi nzima kwa wakati sahihi, na kukamilisha matibabu yote. Dawa hizo hufanya kazi vyema zaidi ili kuzuia kushikwa na ugonjwa amilifu wa TB ikiwa utazitumia ipasavyo.

Aidha, kulingana na chaguo la matibabu, huenda ukahitaji kukutana na mto huduma wako wa afya ili kutumia dawa zako. Haya ni matibabu yanayozingatiwa moja kwa moja (DOT). Matibabu ya DOT yanaweza kuwa yenye manufaa kwa kuwa mto huduma wako wa afya anawenza kujibu maswali, kushughulikia madhara yoyote yanayotokana na tiba, na kuhakikisha kwamba unakamilisha matibabu yako haraka iwezekanavyo.

## **NJIA ZA KUPANGA UZAZI ZILIZO NA HOMONI NA MATUMIZI YA POMBE WAKATI WA MATIBABU YA MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA**

Ikiwa kwa sasa unatumia njia ya kupanga uzazi iliyo na homoni tembe za kupanga uzazi, njia ya kupanga uzazi inayopandikizwa mkononi, kipete cha Nuvaring kinachoingizwa ndani ya uke, inayobandikwa juu ya ngozi, sindano ya depo provera, tembe zilizo na progesterone tu), tafadhali kumbuka kuwa dawa za TB zinaweza kuathiri jinsi dawa hizi zinavyofanya kazi. Tafadhali jadili haya na mto huduma wako wa afya na pia utumie njia za ziada za kupanga uzazi, kama vile mipira ya kondomu, ili kuzuia mimba.

Kunywa vileo, kama vile bia, pombe, au divai, wakati wa kutumia dawa za TB kunaweza kuwa hatari. Tafadhali jadili matumizi yoyote ya vimeo na mto huduma wako wa afya.

## **KWA NINI NITUMIE DAWA IKIWA SIJIHISI MGONJWA?**

Ingawa huenda hujisikii mgonjwa na huwezi kueneza TB kwa wengine, mradi una bakteria za TB katika mwili wako, zina uwezo wa kukufanya uwe mgonjwa. Njia ya pekee ya kuangamiza bakteria za TB ni kukamilisha matibabu yako yote ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara.

## **VIPI IKIWA NITAKOSA KUTUMIA DAWA ZANGU ZA MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA KWA KIPINDI FULANI?**

Ikiwa utasahau kutumia dawa zako za maambukizi ya TB yasiyo na madhara wakati fulani, mfahamishe mto huduma wako wa afya katika miadi yako ijayo. Hakikisha hatumii dawa za ziada, kwa kuwa haiependekezwi kwamba utumie zaidi ya dozi ya dawa uliyoagizwa.

Ikiwa utakosa kutumia dawa zako za maambukizi ya TB yasiyo na madhara kwa muda wa wiki mbili au zaidi, panga miadi ya kuonana na mto huduma wako wa afya haraka iwezekanavyo ili kubaini jinsi utakavyoendelea na mpango wako wa matibabu ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara.

## **JE, DAWA ZINALETA MADHARA?**

Ingawa watu wengi wanaweza kustahimili dawa za matibabu ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara vizuri sana, kuna madhara yanayotokea mara nyingi. Mengi ya madhara haya ni ya kiwango kidogo, lakini mengine huenda yakahitaji matibabu ya haraka. Kulingana na aina ya matibabu uliyopewa, unaweza kushuhudia yafuatayo:

- Mate, mkojo, machozi, na majimaji mengine ya mwili kuwa na rangi ya chungwa yenye wekundu - hali hii ni ya kawaida na inaweza kufifia baada ya muda
- Uchovu

Ikiwa utapata madhara makali wakati wa matibabu yako, tafadhali wasiliana na mto huduma wako wa afya mara moja. Madhara makazi ni pamoja na:

- Kizunguzungu
- Kupoteza hamu ya kula
- Dalili kama za mafua (kwa mfano, homa, kuhisi kijibaridi, maumivu ya kichwa, kizunguzungu, maumivu ya mfumo wa mifupa ya na misuli)
- Kuharisha sana au kinyesi chenye rangi nyepesi
- Kupungukiwa na pumzi
- Hisia za huzuni au msongo wa mawazo
- Homa
- Kupoteza uzito wa mwili bila sababu
- Mkojo wa kahawia (rangi ya kahawa au cola)
- Ngozi au macho yenye rangi ya manjano
- Vipele
- Kuhisi mchonyoto kwenye mikono na miguu
- Uchovu au udhaifu wa unaodumu kwa siku 3 au zaidi
- Maumivu ya tumbo
- Kuvilia au kutokwa na damu kwa urahisi
- Maumivu ya maungo
- Kichefuchefu
- Kutapika
- Kuwashwa

## **NI NINI KINACHOWEZA KUTOKEA NISIPOKAMILISHA MATIBABU YANGU?**

Ikiwa hutakamilisha matibabu yako yote ya dawa za maambukizi ya TB yasiyo na madhara, bakteria za TB zitabakia katika mwili wako na zinaweza kugeuka kuwa ugonjwa amilifu wa TB. Kwa mara nyingine, njia ya pekee ya kuangamiza bakteria za TB ni kukamilisha matibabu yako yote ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara.

## **NI NINI KITAFANYIKA BAADA YA KUKAMILISHA MATIBABU YANGU?**

Mara baada ya kukamilisha matibabu yako ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara, utapokea hati za kuthibitisha kukamilisha matibabu kutoka kwa mto huduma wako wa afya. Hati hizi zitakuwa ni pamoja na matokeo ya vipimo vya TB, matokeo ya picha ya eksirei ya kifua, majina, dozi, na muda wa kutumia dawa zako za matibabu, na taarifa za mto huduma wako wa afya.

Hakikisha kwamba utaweka hati hizi mahali salama, kwani utahitaji kuziwasilisha katika siku zijazo wakati wowote ambapo ukaguzi wa TB unaombwa. Kwa kuwa vipimo vingine vyovoyote vya TB vya baadaye vitakuwa na matokeo chanya, huhitaji kupimwa TB hapo baadaye. Hata hivyo, daima hakikisha kuwa makini ili kutambua dalili zozote za ugonjwa amilifu wa TB zilizotajwa hapo awali. Mpigie simu mto huduma wako wa afya ikiwa utashuhudia dalili zozote za ugonjwa amilifu wa TB.



Chuo Kikuu cha Huduma za Afya cha Brown. (2019). *Matibabu ya Maambukizi ya TB Yasiyo na Madhara (LTBI): Msururu wa Mafundisho ya Wagonjwa wa Huduma za Afya za Brown*. Huduma za Afya za Chuo Kikuu cha Brown. <https://www.brown.edu/campus-life/health/services/sites/brown.edu.campus-life.health.services/files/LTBI%20Treatment.pdf>

Idara ya Afya ya Umma ya California. (2018). *California Isiyo na TB: Kuzungumza na wagonjwa wako kuhusu maambukizi ya TB yasiyo na madhara (watu wazima)*. Idara ya Afya ya Umma ya California. [https://www.cdph.ca.gov/Programs/CID/DCDC/CDPH%20Document%20Library/Latent%20TB%20Starter%20Kit%20for%20Providers/Provider\\_script\\_for\\_LTBI\\_counseling-adults.pdf](https://www.cdph.ca.gov/Programs/CID/DCDC/CDPH%20Document%20Library/Latent%20TB%20Starter%20Kit%20for%20Providers/Provider_script_for_LTBI_counseling-adults.pdf)

Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa. (2012). *Kifua Kikuu: Pata Ukweli!* [Brosha]. [https://www.cdc.gov/tb/publications/pamphlets/Tuberculosis\\_Get\\_the-facts.pdf](https://www.cdc.gov/tb/publications/pamphlets/Tuberculosis_Get_the-facts.pdf)

Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, Kituo cha Kitaifa cha Kuzuia VVU/UKIMWI, Virusi vya Homa ya Ini, Magonjwa ya Zinaa, na TB, Kitengo cha Kuangamiza Kifua Kikuu. (2020). *Maambukizi ya Kifua Kikuu Yasiyo na Madhara: Mwongozo kwa Watoa Huduma za Afya wa Msingi*. Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa. <https://www.cdc.gov/tb/publications/faqs/pdfs/qa.pdf>

Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, Kituo cha Kitaifa cha Kuzuia VVU/UKIMWI, Virusi vya Homa ya Ini, Magonjwa ya Zinaa, na TB. (2014). *Maswali na Majibu Kuhusu Kifua Kikuu [TB]*. Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa. <https://www.cdc.gov/tb/publications/faqs/pdfs/qa.pdf>

Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, Kituo cha Kitaifa cha Kuzuia VVU/UKIMWI, Virusi vya Homa ya Ini, Magonjwa ya Zinaa, na TB. (2014). *TB: Unachohitaji Kujua Kuhusu Maambukizi ya Kifua Kikuu*. Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa. [https://www.cdc.gov/tb/publications/pamphlets/tb\\_infection.pdf](https://www.cdc.gov/tb/publications/pamphlets/tb_infection.pdf)


Kituo cha Kimataifa cha Kifua Kikuu cha Curry. (Agosti 2020). *Maambukizi ya TB Yasiyo na Madhara "TB Iliyodumaa"* [Slaidi za PowerPoint]. Kituo cha Kimataifa cha Kifua Kikuu cha Curry. <https://www.currytbcenter.ucsf.edu/products/ltdi-flipbook-patient-education-tool>

Sterling, T.R., Njie, G., Zenner, D., Cohn, D.L., Reves, R., Ahmed, A., Menzies, D., Horsburgh Jr, C.R., Crane, C.M., Burgos, M., LoBue, P., Winston, C.A., na Belknap, R. (2020). Miongozo ya Matibabu ya Maambukizi ya Kifua Kikuu Yasiyo na Madhara: Mapendekezo kutoka kwa Chama cha Kitaifa cha Wadhibiti wa Kifua Kikuu na CDC, 2020. *Taarifa ya Kila Wiki ya Viwango vya Visa vya Ugonjwa na Maafa* (MMWR): Mapendekezo na Taarifa, 69(Nambari RR-1), 1-11.DOI: <http://dx.doi.org/10.15585/mmwr.rr6901a1>

# VIDOKEZO

# VIDOKEZO

**VIDOKEZO**



**Latent TB. Active Concern.  
Tuberculosis Program**

*Mpango wa TB wa Idara ya Afya ya Virginia unalenga kuzuia, kutibu,  
na kuangamiza TB ili kulinda afya na kukuza ustawi wa watu wote katika Virginia.*

*Kwa taarifa zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu ya  
<https://www.vdh.virginia.gov/tuberculosis/>  
au uwasiliane nasi kupitia 804-864-7906 au [tuberculosis@vdh.virginia.gov](mailto:tuberculosis@vdh.virginia.gov)*